**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA**


Shule ya Sekondari Tanga Ufundi
S.L.P 5002
**TANGA**

SIMU NA: 0789 589 472/0654 488483 - MKUU WA SHULE
0784 688 916/0735 688 916 - MAKAMU M/SHULE
0714 636 489 - PATRON

Tovuti: www.tangaschool.sc.tz
Barua pepe: tangaschool@yahoo.com


Kumb. Na. TTS.E./V/2025/2026 **02/06/2025**

Kwa: ……………………………………………
……………………………………………
……………………………………………
……………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS)**
**KIDATO CHA TANO 2025/2026 – TANGA SCHOOL**

1.0 Ninayo furaha kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako **kujiunga** na Shule hii katika kidato cha **TANO 2025 /2026.** **KARIBU SANA TANGA SCHOOL** (Shule ya Sekondari ya kwanza ya Serikali) nchini. Ni shule ya bweni kwa kidato cha kwanza hadi cha sita. Pia ni shule ya mchepuo wa Ufundi na mchanganyiko wa wasichana na wavulana kwa kidato cha Kwanza hadi cha Nne. Aidha, ni shule yenye Tahasusi za Sayansi ("Subject Combinations") **PCB, PCM** & **PMCs** kwa Kidato cha Tano na Sita.
Nina imani kwamba utafurahi/utafaidika kusoma katika shule hii yenye sifa nyingi.
Shule itafunguliwa **08/07/2025 .** Mwisho wa kuripoti **21/07/2025.**
Shule iko katika **Jiji la Tanga, eneo la Makorora** karibu na **Makorora Community Centre Kilometa 10 kutoka Kituo Kikuu cha Mabasi Kange**. Kuna usafiri wa Town Bus: Kange – Stand= **600/=** Stand-Sahare au Donge=**600/=**

=====================================================

2.0 **MALAZI**

Mwanafunzi anatakiwa awe na **godoro jipya** la sponge ft. 2 ½ la inchi nne (ikiwezekana liwe na waraka) aidha godoro linaweza kupatikana maeneo ya shuleni kwa gharama ya **Tshs 40,000**/=, **shuka mbili** rangi ya pinki na **neti ya kuzuia mbu**, foronya na mto. Mwanafunzi atapangiwa Bweni na Darasa katika Ofisi ya Makamu wa Mkuu wa Shule. Ni **MARUFUKU** kwa Mwanafunzi yeyote, kukaribisha Mgeni Bwenini, bila KIBALI cha Uongozi wa Shule.

=====================================================

3.0 **SARE ZA SHULE**

Mwanafunzi aje na:-

- Suruali rangi Nyeusi Jozi mbili (2) - **Kitambaa Kimeambatanishwa**
- Suruali rangi ya Khaki Jozi mbili (2)- Shamba Dress (**Kitambaa Kimeambatanishwa**)
- Shati rangi Nyeupe Jozi mbili (2) mikono mifupi
- Fulana rangi ya Kijivu Jozi mbili (2)- Shamba Dress zenye Nembo ya Shule,
- Shuka rangi ya Pinki Jozi mbili (2),
- Viatu vyeusi vya ngozi Jozi mbili (2), siyo buti na visiwe na visigino virefu,
- Soksi rangi nyeusi Jozi mbili (2),
- Mkanda mweusi wa Ngozi wenye kifungio cha Kawaida.

**NB: Vitu hivi awe navyo muda wote awapo shuleni ili kuepuka usumbufu.**

**Vifaa vya michezo**: Raba au viatu vyovyote vya michezo, T. Shirt na Bukta au "**track suit**" rangi ya **"light blue".** Pia

**NB: Kama utahitaji Huduma ya Fundi wa Kushona Nguo, karibu na Shule (kwa ajili ya Udhibiti wa Mishono sahihi) Gharama za Sare hizo ni kama ifuatavyo:**

- Tshs.36,000/= kwa ajili ya Suruali Nyeusi Jozi mbil (**2**),
- Tshs. 36,000/= kwa ajili ya Suruali Khaki Jozi Mbili(**2**),
- Tshs.20,000/= kwa ajili ya Shati Nyeupe Jozi mbili (**2**),
- Tshs.16,000/= kwa ajili ya Shuka Rangi ya Pinki Jozi mbili (**2**),
- Tshs. 5,000/= kwa ajii ya Muhuri/alama kwenye nguo zake zote
- Tshs. 15,000/= kwa ajili ya Jezi na Bukta Jozi (**1**) (**Light Blue**)
- Tshs. 25,000/= kwa ajili ya Truck Suit Jozi (**1**) (**Light Blue**)

Tshs. 25,000/= kwa ajili ya Tshirt yenye Nembo ya Shule Jozi Mbili (**2**) (**Fulana rangi ya Kijivu)**

3.1 **Nyongeza**

- Vifaa vingine vya matumizi binafsi vinaruhusiwa kama kawaida mfano: - Taulo, Chandarua, (**chandarua ni lazima**) ndoo ya kufulia, yeboyebo nyeusi kwa ajili ya kufanyia kazi za nje nk.
- Unaweza kupata maeneo ya Shule kwa Tshs. 15,000/= Tshirt na Bukta au Tshs. 25,000/= Track suit za rangi ya 'Light Blue'

**3.2 Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa suruali zinazobana (vimodo), vikoti, makoti, vilemba, kofia, vizibao, bangili, mkufu na mapambo kama sehemu ya sare ya shule.**

*** Suruali chini ziwe na upana wa inchi 17 au 18, mbele iwe na rinda mbili ("celebration") kila upande na mifuko miwili ya "cross", na nyuma iwe na mfuko mmoja. Aidha, inatakiwa iwe na luksi sita za kuwekea mkanda**

- Mzazi ambaye anafikiri mtoto wake hawezi sharti la **MAVAZI** hapa shuleni anashauriwa AFANYE UTARATIBU MTOTO WAKE AHAMIE SHULE NYINGINE.

3.3 Usafi wa mwili na mavazi yote yanayoruhusiwa kuvaliwa hapa shuleni ni muhimu. Ukaguzi utafanywa mara kwa mara kuthibitisha usafi huo.

3.4 Uvaaji wa Sare ni **lazima kwa wanafunzi** wote wakati wa:-

(a) Masomo darasani

(b) Wanafunzi wanapotoka nje ya shule

(c) Mhadhara wa Shule (BARAZA)

(d) Maandamano

(e) Mikutano

(f) Mahafali ("Graduation")

3.5 Mwanafunzi atatakiwa kuvaa Suruali ya Khaki na Fulana ya Kijivu (Shamba Dress) awapo katika eneo la shule nje ya muda wa vipindi vya kawaida vya Darasani **na SI VINGINEVYO.**

3.6 Sweta sio sehemu ya sare ya shule ya sekondari Tanga Ufundi. Kama mwanao atalazimika kuvaa sweta shuleni kwa sababu za kiafya **zilizothibitishwa na Daktari**, Sweta inayokubalika ni ile yenye rangi ya "Dark Blue" yenye shingo **V.**

====================================================

4.0 **MAHITAJI YA FEDHA AU VIFAA**

Kila mwanafunzi anatakiwa aje na mahitaji yafuatayo:-

4.1 **MICHANGO MBALIMBALI**

| NA. | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho | 5,000/= |
| **JUMLA** | | **80,000/=** |

**NB**: Fedha zote, zilipwe kupitia Akaunti ya Shule – NMB.
Jina la Akaunti ni: **TANGA SCHOOL FUND. A/C No. 4170 6600 080.**

**Ni lazima Bank-Pay-In-Slips (BPS) iwasilishwe shuleni ili mwanafunzi apatiwe risiti.**
**BPS hiyo ionyeshe majina ya mwanafunzi na SIO MZAZI/MLEZI.**
**Fedha za nguo zilizotajwa zisiwekwe benki, ziwe "Cash"**
****USILIPE FEDHA YA NGUO BENK.**

4.2 **MAHITAJI MENGINE MUHIMU:**

(i) **Nakala za Cheti cha Kuzaliwa na Hati ya Matokeo k4 (Result Slip)**
(ii) Ream 2 za karatasi (1 'photocopy') & nyingine (1 'ruled')
(iii) Sanduku la Bati na Ndoo kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi
(iv) Fedha/Vifaa muhimu k.v. nauli ya kurudia nyumbani/Maths Set/Fedha za matumizi madogo madogo/vyombo vya chakula. Madaftari/kalamu/" Graph papers", chandarua nk.
**NB**: **Mwanafunzi aweke Fedha za ziada kwenye Akaunti yake Benki.**
(v) Picha 4 (Pass Port size) zipigwe na sare ya shule - zinaweza kupatikana shuleni kwa gharama ya Tshs. 3,000/=
(vi) Vitabu vya Masomo ya Tahasusi husika (Orodha imeambatanishwa), Na madaftari ya masomo Q3 au Q4
(vii) Dissecting Kit kwa wanafunzi wa Biology,
(viii) 'Non-Programmable Scientic Calculator' (fx 991),
(ix) Stop Watch kwa ajili ya maabara
(i) Vifaa vya usafi vifuatavyo: Fyekeo 1(wote); Fagio la Chelewa lenye mpini 1(PCM), Soft broom (PCB) na Jembe lenye mpini (wote). Vifaa hivi vinaweza kupatikana maeneo ya shuleni kwa gharama ya fyekeo 5,000/=, Jembe na mpini 10,000/= na fagio la chelewa 3,000/=
(ii) Vyombo vya kulia chakula na kunywea uji na malapa. (vinaweza pia kupatikana dukani shuleni)

==================================================

5.0 **MIPAKA YA SHULE**

(i) Mipaka ya shule iko wazi na utakapofika hapa utaiona/utaonyeshwa
(ii) Hairuhusiwi kutoka nje ya mipaka hiyo bila kibali cha Mkuu wa Shule
(iii) Saa za kutoka nje ya mipaka hiyo zimeonyeshwa kwenye ratiba ya siku ya Jumapili.

6.0 Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum

(a) Chumba maalum cha walimu (Staff room)
(b) Ofisi za shule (school offices)
(c) Maabara na karakana
(d) Jikoni
(e) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu

7.0 **SEHEMU AMBAZO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUONEKANA**

**Ni marufuku** kuonekana sehemu zifuatazo:-

(a) Vilabu vya pombe (Bars, Night Clubs, Vigodoro)
(b) Majumba ya Starehe (Cinema Halls, Disco Halls nk)
(c) Majumba ya kufikia wageni (Guest Houses)

8.0 **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII:**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla, ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
(c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kufanya hivyo.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

8.1 **MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

(a) WIZI
(b) UASHERATI/UBAKAJI/ULAWITI/USHOGA
(c) ULEVI WA AINA YOYOTE
(d) UVUTAJI WA SIGARA/BANGI/UTUMIAJI WA DAWA ZA KULEVYA
(e) MAKOSA YA JINAI
(f) KUPIGANA AU KUPIGA
(g) KUHARIBU MALI YA MTU/ UMMA/FEDHA YA SERIKALI KWA MAKUSUDI,
(h) KUDHARAU BENDERA YA TAIFA/VIONGOZI WA SERIKALI,
(i) KUOA AU KUOLEWA
(j) KUPATA MIMBA/KUMPA MWANAMKE MIMBA
(k) KUSHIRIKI MATENDO YA UHALIFU, SIASA NA MATENDO YOYOTE YALE YANAYOVUNJA SHERIA ZA NCHI,
(l) KUTEMBELEA MAJUMBA YA STAREHE NA NYUMBA ZA KULALA WAGENI,
(m) KULALA NJE YA SHULE BILA KIBALI CHA MKUU WA SHULE
(n) KUTOA MIMBA/KUSHIRIKI KATIKA KUTOA MIMBA
(o) KUTOHUDHURIA VIPINDI VYA DARASANI KWA ZAIDI YA SIKU 90 BILA TAARIFA/UTORO,
(p) KUTOA LUGHA CHAFU KWA WANAFUNZI WENZAKE, WALIMU/WALEZI NA JAMII KWA UJUMLA,
(q) KUFUGA NDEVU AU NYWELE NDEFU,
(r) KUGOMA, KUCHOCHEA, KUONGOZA AU KUVURUGA AMANI NA USALAMA WA SHULE AU WATU,
(s) KUFANYA JARIBIO LOLOTE LA KUJIUA, AU KUTISHIA KUJIUA KAMA KUNYWA SUMU N.K.
(t) KUKATAA ADHABU KWA MAKUSUDI,
(u) KUTOKA NJE YA SHULE BILA SARE YA SHULE AU BILA KIBALI,
(v) KUMILIKI, KUKUTWA AU KUTUMIA SIMU YA MKONONI/LINE YA SIMU/CHARGER KATIKA MAZINGIRA YA SHULE.

## 9.0 MAENEO YA KUFANYA KAZI

### 9.1.0 Mabwenini

9.1.1 Kila mwanafunzi atapangiwa na mwalimu wa bweni eneo la kufanya kazi asubuhi na jioni baada ya saa za darasani.

9.1.2 Hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mwanafunzi atakayeacha kuhudumia eneo lake kikamilifu. Aidha kila asubuhi/jioni mwanafunzi anatakiwa kufanya usafi katika bweni, bwalo,maeneo nk. Kama atakavyopangiwa na mwalimu/viongozi wake.

9.1.3 Ni **marufuku** kuwa bwenini wakati ambapo mwanafunzi anatakiwa kuwa darasani/miradi/michezo/Roll-check/Baraza/Mahafali nk.

### 9.2.0 Darasani

9.2.1 Wanafunzi wote wanatakiwa wawe madarasani
Kuanzia saa 1:30 – 4:50, 5:20 – 6:40, 7:00 – 9:00 alasiri.
Saa 2:00 – usiku – 5:00 usiku. Aidha, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa darasani siku ya Jumamosi Saa 3:00 asubuhi-Saa 6:30 Mchana na Siku ya Jumapili kuanzia Saa 8:00 mchana hadi saa 10:00 jioni kwa ajili ya kujisomea.

9.2.2 Darasa liwe safi (lisiwe na buibui, vumbi, karatasi nk) Mwalimu wa Darasa atakagua vyumba vya madarasa mara kwa mara. Kiongozi wa darasa na kiranja wahakikishe kila darasa ni safi.

9.2.3 Wakati mwanafunzi akiwa darasani anatakiwa afanye yafuatayo:-

(i) Mwanafunzi asipige kelele/asitoketoke darasani

(ii) Mwanafunzi aulize na kujibu maswali

(iii) Mwanafunzi afanye test/mazoezi/majaribio yote kwa uwezo wake wote. Kila mwanafunzi awe na daftari la mazoezi/test kwa kila somo.

(iv) Viti/madawati yapangwe kwenye mistari iliyonyooka

(v) Mwanafunzi **analazimika** kuhudhuria vipindi vyote kwa siku.

(vi) "Private Study" iliyopo kwenye ratiba ya siku hiyo ni **lazima** ifanyike darasani.

(vii) Ni marufuku kuhamisha kiti/dawati/taa/switch n.k. kutoka darasa moja kwenda mahali pengine. Viongozi wa wanafunzi (monita na viranja) wahakikishe kwamba hakuna kifaa kilichohamishwa kutoka darasa moja kwenda mahali bila kibali cha mwalimu wa darasa. Aidha, ni marufuku kwa mwanafunzi kuchafua/kuchora kuta/samani za shule, kuchezea na kuharibu miundombinu ya umeme na maji shuleni.

## 10.0 CHAKULA

Shule inaandaa Chakula kwa ajili ya Wanafunzi wote kila Siku.Kila Mwanafunzi **ni lazima** ale chakula hicho kinachoandaliwa na shule. Chakula kiliwe ndani ya Bwalo, na ni marufuku kupeleka chakula Bwenini au mahali pengine popote nje ya Bwalo bila KIBALI maalum. **Aidha, Hakuna Mwanafunzi anayeruhusiwa kutoka nje ya Mipaka ya Shule kwa ajili ya kutafuta Chakula.**

## 11.0 UTAMADUNI NA MICHEZO

### 11.1.0 Michezo

11.1.1 Shule ina michezo kama vile mpira wa miguu, wavu, kikapu, pete, meza, riadha, kuruka juu/chini na Sarakasi. Kila mwanafunzi ni **LAZIMA** ashiriki kikamilifu katika angalau mchezo mmoja. Utaratibu umeandaliwa na Mratibu wa michezo na Mwalimu Mwandamizi Malezi & Utamaduni.

11.1.2 Mwanafunzi ambaye hawezi kushiriki katika michezo hiyo awe na barua ya daktari na apewe kibali na Mkuu wa Shule.

11.1.3 Mashindano yatafanyika kila muhula na zawadi zitatolewa kwa washindi

11.1.4 **Kutakuwa na Mchakachaka kila Jumamosi saa 11:45 asubuhi isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo na Uongozi wa Shule.**

=====================================================

12.0 **HUDUMA MUHIMU**

12.1.0 **MATIBABU**: Shule ina Zahanati inayohudumiwa na Nesi. Kila mwanafunzi mwenye tatizo la afya yake aingiapo shuleni atoe taarifa kwa Nesi wa Zahanati kama vile Pumu, Pressure, Kisukari, Vidonda vya tumbo nk.

12.1.1 Mwanafunzi haruhusiwi kuweka dawa bwenini. Dawa zote zikabidhiwe Zahanati ambapo mwanafunzi atapewa dawa kwa kiasi/kiwango kinachojulikana na mtaalamu wa afya.

12.1.2 Matibabu yanatolewa kwenye Zahanati ya shule kwa utaratibu utakaoelekezwa na Uongozi wa Shule. Aidha, **kila Mwanafunzi, anatakiwa awe na Kadi ya Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF), ili kupanua Wigo wa Huduma za Afya katika Hospitali za Rufaa; ili kuepuka usumbufu kama mwanao hana bima anatakiwa awe na shilingi elfu hamsini na mia nne (50,400) kwa ajili ya BIMA ya wanafunzi (Gharama za Matibabu nje ya Zahanati ya Shule, zitagharamiwa na Mzazi/Mlezi kama hana BIMA).**

12.2.0 **Hospitali za "Rufaa"**

12.2.1 Mwanafunzi atakayepata huduma katika Zahanati ya shule na kugunduliwa kwamba anahitaji huduma ya ziada atapelekwa kwenye Kituo cha Afya Makorora au Hospitali ya Rufaa ya Mkoa (Bombo Regional Hospital) na atatumia Kadi ya Bima ya Afya au gharama binafsi toka kwa mzazi/mlezi wake.

12.2.2 Mwanafunzi atakayezidiwa mzazi/mlezi atapewa taarifa kwa hatua zaidi.

12.3.0 **KUABUDU**

12.3.1 **MSIKITI**

Kuna Msikiti wa Shule kwa ajili ya Wanafunzi wa Kiislamu. Msikiti huo upo hapa shuleni, kwa ajili ya Kuswali. Ni marufuku kutumia Msikiti huo kwa ajili ya **Makazi** ya Wanafunzi au Wageni.

12.3.2 **MAKANISA**

Madhehebu mengine wana utaratibu wa kusali nje kwenye makanisa yaliyokaribu na Shule.

12.3.3 Vipindi vya dini – kuna vipindi viwili kwa wiki ambavyo hutolewa hapa shuleni kwa madhehebu yote. **NI LAZIMA** kila mwanafunzi ahudhurie vipindi hivyo viwili vya dini.

12.4.0 **HAKUNA SIKU YA KUTEMBELEA WANAFUNZI ISIPOKUWA SIKU YA MAHAFALI AU UTAKAPO TAARIFIWA NA UONGOZI WA SHULE.**

13:0 **MITIHANI**

Kila muhula wanafunzi wanafanya mitihani na matokeo kutumwa kwa wazazi kwa njia ya Mtandao. Tovuti ya Shule ni www.tangaschool.sc.tz. Mtoto wako ajitahidi asipate wastani wa alama **CHINI YA 50%** ukipata chini ya wasitani huu mzazi ataitwa shule kwa majadiliano.

Kama wewe Mzazi/Mlezi hupati matokeo ya mitihani ya mwanao (kila muhula), wasiliana na Shule haraka iwezekanavyo.

14.0 **KURUDI SHULENI BAADA YA LIKIZO**

Ni jukumu la mzazi kuona kwamba mwanao anarudi shuleni siku angalau moja kabla ya siku ya kufunguliwa shule. Shule ikishirikiana na Bodi ya shule wana mikakati ya kuimarisha elimu ambapo mwanafunzi

atakayechelewa kurudi kutoka likizo fupi au ndefu kwa siku moja au zaidi itabidi **AJE NA MZAZI/MLEZI WAKE**. Mwanafunzi ambaye hatakuja na **MZAZI/MLEZI HATAPOKELEWA SHULENI**. Kama kuna tatizo la kiafya wasiliana na uongozi wa shule kabla ya siku ya kufungua shule.

**UKOSEFU WA MICHANGO HAUTAKUBALIKA KWAMBA NI SABABU YA KUCHELEWA KUJA SHULENI.**

15.0 **MENGINEYO**

15.1 **MUHIMU KWA MZAZI**

(i) Mchango **WOWOTE** utakaotakiwa na shule kutoka kwa Mzazi, ni lazima uwe kimaandishi pamoja na Saini na muhuri wa Mkuu wa Shule. Kinyume cha hapo usimpe mwanao mchango ambao hauna barua.

(ii) Tabia na mwenendo wa mtoto wako akiwa likizo ni **JUKUMU LAKO** na tutafurahi sana kama utatuandikia kuhusiana na tabia ya mtoto wako alipokuwa likizo, mema/mabaya aliyofanya, ushauri uliompa mwanao pamoja na tarehe aliyotoka nyumbani kurudi shuleni. Maelezo haya yatatusaidia sana katika malezi ya mwanao.

(iii) Mzazi afuatilie sana utekelezaji wa Vipengele 13:0 & 14:0 hapo juu.

(iv) **Mwanafunzi asije na Redio, Simu ya mkononi (Cellular phone)/charger/line na vifaa vyote vinavyotumia umeme.**

15.2 **MUHIMU KWA MWANAFUNZI**

(a) Hutapokelewa shuleni kama hukukamilisha kipengele 2.0, 3.0 & 4.0 hapo juu.

(b) **"JIHESHIMU NAWE UTAHESHIMIWA"**

(c) **Fomu zilizoambatanishwa zijazwe kikamilifu na Wahusika na kuletwa shuleni. Mwanafunzi hatapokelewa, kama hataleta nakala ya cheti cha kuzaliwa au uthibitisho wowote wa Uraia wa Mwanafunzi, na kujaza Fomu ya Hospitali na Historia ya mwanafunzi. Fomu ya hospitali iwe na karatasi ya Risiti ya malipo ya serikali.**

**MUHIMU SANA:**
Kama Mwanafunzi HUKUBALIANI na MASHARTI yaliyotajwa hapo juu **USIJE SHULENI** ila **MZAZI/MLEZI** atafute UHAMISHO wako kwenda shule nyingine. Mwanafunzi anayekuja hapa shuleni baada ya kusoma taratibu za shule hii **HATEGEMEWI KUVUNJA SHERIA/KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE.**
Kwani akifanya hivyo, ni kwa **MAKUSUDI** na **SIYO BAHATI MBAYA**.

**N.B: 1. Endapo Mwanafunzi atachelewa kuripoti shuleni hadi** tarehe **21/07/2025 ambayo ndio siku ya mwisho ya kuripoti, nafasi yake atakuwa ameipoteza na itachukuliwa na mwanafunzi mwingine aliyekosa nafasi.**

**N.B: 2.** Kwa siku za hivi karibuni kuwekuwa na utapeli (**wizi kwa njia ya mitandao**). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. **TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZA SIMU ZILIZOPO JUU UKURASA WA 1.**

.................................... HEADMASTER TANGA TECHNICAL SCHOOL TANGA
M.M. LUZILO
HEADMASTER

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Nakala: | (i) | Katibu Mkuu,<br>OR – TAMISEMI,<br>S.L.P 1923,<br>DODOMA. | - | Taarifa |
| | (ii) | Katibu Mkuu<br>Wizara ya Elimu, Sanyansi na Tekinolojia<br>S.L.P 10<br>DODOMA. | | |
| | (iii) | Maafisa Elimu wa Mikoa (Tanzania Bara) | - | Taarifa |
| | (iv) | Mkaguzi Mkuu wa Shule (K)<br>Kanda ya Kaskazini Mashariki<br>MOSHI | - | Taarifa |
| | (v) | Afisa Elimu Sekondari,<br>S.L.P 178<br>TANGA | - | Taarifa |
| | (vi) | Wajumbe wa Bodi ya Shule | - | Taarifa |
| | (vii) | Faili la Shule | | |

**FORM A**
**TANGA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL**
P.O. BOX 5002
**TANGA**
**02.06.2025**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**PART A**

To: Medical Officer
………………………………………………
………………………………………………
………………………………………………

RE: MR/MISS……………………………………………………………………………………………
(Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time school course. The examination should include the following categories (I – III) each category or sub-category of which will render the applicant in-eligible in case of defect. Pregnancy (category (IV) will also render a girl candidate ineligible for the course.

I. (a) Eye-sight
(b) Hearing
(c) Limbs
(d) Speech
(e) Venereal Disease(s)
(f) Leprosy
(g) Epilepsy

II. Neuroses

III. Other serious diseases(s)

………………………………
M.M. LUZILO
HEADMASTER

HEADMASTER
TANGA TECHNICAL SCHOOL
TANGA

---

**PART B**
**MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by Government Medical Officer)
I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time school course.

i. (a) Eye-Sight………………………………………… (b) Hearing……………………..
(c) Limbs…………………………………………….. (d) Speech………………………
(e) Venereal Diseases…………………………… (f) Leprosy……………………..
(g) Epilepsy…………………………………………..

ii. Neuroses…………………………………………
iii. Other Serious Disease(s)…………………
iv. Pregnancy test…………………………………

Signature…………………………………………….Station……………………………………

Designation……………………………..Date ........................*Delete as necessary

**FOMU B**

**SHULE YA SEKONDARI TANGA UFUNDI**

**HISTORIA YA MWANAFUNZI (Ijazwe na Mwanafunzi)**

1. (i) Jina la mwanafunzi…………………………………………………………………………………………………
(**NB**. Jina hili ni **LAZIMA** liwe lile la kwenye **F4 SEL-FORM au CSEE** na libaki hivi kwa kipindi chote utakachokuwa katika Shule hii).

Shule atokayo……………………………………………………………………………….………………………..

(ii) Tarehe ya kuzaliwa……………………………Wilaya………………....Mkoa…….….………………………

(iii) Dini……………………………………………Dhehebu……………………………………

(iv) Shule ulizosoma kabla ya kuja Sekondari ya Tanga Ufundi

| JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI | SHULE YA MSINGI/SEKONDARI | KIPINDI ULICHOSOMA |
|---|---|---|
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |

Saini ya Mwanafuzi………………………………………………………………………..

2. **AFYA**

(i) Taja magonjwa yoyote makubwa uliowahi kuugua mfano:TB, Polio, Kifafa nk.

……………………………………………………………………………………………………….

(ii) Taja matatizo ya afya yako……………………………………………………………………

3. **JINA LA MZAZI**

(i) Mama……………………………………………………*Hai/amefariki lini…......................?

(ii) Baba…………………………………………………*Hai/amefariki lini… .........................?

**KAZI YA**

(iii) Baba…………………………………dini…………………………dhehebu………………………

(iv) Mama……………………………….dini………………………..dhehebu………………………

(v) Anuani ya Mzazi kwa sasa: S.L.P………………wilaya………………..mkoa…………………

4. (i) Jina la atakayegharamia mahitaji ya shule…………………………………………………………

(ii) Kazi yake ni………………………………………………………………………………………..

(iii) Anuani yake ni: S.L.P…………….….. wilaya……….……………..mkoa……………………

(iv) Uhusiano… .......................................... (mf. Kaka, Dada, Mjomba, Baba, Mama nk)

(v) Dini yake……………………………………..Dhehebu……………………………………………

(vi) Namba ya Simu ya Mzazi/Mlezi

- Jina……………………………………Namba ya Simu…………………….Uhusiano……………
- Jina……………………………………Namba ya Simu…………………….Uhusiano……………
- Jina……………………………………Namba ya Simu…………………….Uhusiano…………….
- Jina……………………………………Namba ya Simu…………………….Uhusiano…………….

5. **Uthibitisho wa mwanafunzi**

Mimi .................................................................................. ninakiri kuzisoma na kuzielewa taratibu/sheria za Shule ya Sekondari Tanga Ufundi, hivyo ninakubali kwa hiari yangu, kujiunga na shule ya Ufundi Tanga na kuthibitisha kuwa nitafuata Sheria na taratibu zote za shule hii, ili nitimize lengo la kuja kwangu hapa kwa manufaa yangu/familia na taifa kwa ujumla. Endapo nitakuwa kinyume na sheria/taratibu za shule nitakubali kuadhibiwa. Naahidi **kutokuchelewa** kurudi shuleni baada ya likizo fupi na ndefu.

Saini ya mwanafunzi……………………………………………………Tarehe………………………

6. **Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi**

Mimi……………………………………………………………………ninakiri kuzisoma na kuzielewa taratibu/sheria za Shule ya Sekondari Tanga Ufundi, hivyo ninathibitisha kuwa nitatoa gharama zote za shule pamoja na mahitaji mengine, kwa lengo la kumwezesha Mwanafunzi aliyetajwa hapo juu asome katika mazingira mazuri kwa kipindi chote atakachokuwa hapo shuleni, kwa kuzingatia sheria na taratibu za shule ya Ufundi Tanga. Aidha nathibitisha kwamba yaliyoandikwa hapo juu ni sahihi. Naahidi kwamba mtoto wangu hatachelewa shule kwa kukosa mahitaji (ada, michango nk)

Saini ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………Tarehe……………………………

NB: Mzazi/Mlezi anayejaza kipengele Namba 6 hapo juu, ndiye atakayetambuliwa rasmi na Shule katika mawasiliano ya aina yoyote. Mabadiliko yoyote yawasilishwe shuleni kimaandishi na Mzazi/Mlezi wa awali, kupitia kwa Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji/Kata.

*Kata isiyohusika.

(*) ***AIDHA, INASISITIZWA KUWA, FOMU HII NI LAZIMA IJAZWE KIKAMILIFU, NA MWANAFUNZI AJE NAYO SHULENI NA KUIKABIDHI FOMU HII, IKIAMBATANA NA FOMU A (MEDICAL EXAMINATION) NA NAKALA YA CHETI CHAKE CHA KUZALIWA KWA MAKAMU MKUU WA SHULE, WAKATI WA UDAHILI.***

## HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA
### SHULE YA SEKONDARI TANGA UFUNDI
### ORODHA YA VITABU A-LEVEL

| SN | SOMO | VITABU |
|---|---|---|
| 1. | PHYSICS | 1. Advanced Level Physics **7th Ed** By **Nelkon & Parker**<br>2. Principles of Physics for class **XI** By S**. Chandy.**<br>3. Principles of Physics for class **X**II By **S. Chandy**. |
| 2. | CHEMISTRY | 1. Conceptual Chemistry for class XI By Dr. **S.K. JAIN**.<br>2. Physical Chemistry By **Ngaiza**.<br>3. Organic Chemistry By **Ngaiza.**<br>4. Inorganic Chemistry By **Ngaiza**.<br>5. Soil Chemistry By **Ngaiza**.<br>6. Principles of Chemical reactions By **Chandy**. |
| 3. | BIOLOGY | 1. Biological Science **3rd Ed** By D.J. Taylor.<br>2. Understanding Biology for Advanced Level By **Glenn** and **Susan Todle.**<br>3. Biology for Advanced Level **By Chandy.**<br>4. Biology for Advance Level Secondary School Form V & VI By **TIE** |
| 4. | ADVANCED MATHS | 1. Pure Mathematics **1** & **2** By **J.K Back House**.<br>2. Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schoosl form **V** & **VI** By **Septine I. Sillem** |
| 5. | BAM | 1. Basic Applied Mathematics for Secondary Schools Form **V** & **VI** By **Septine I. Sillem**. |



